
*KISWAHILI - "Who will deliver me?"*

# NI NANI ATAKAYENIOKOA ?

Jumapili moja nilikuwa nikihubiri Injili ya ajabu katika kijiji kikubwa cha mfalme wa Basutoland, huko Afrika Kusini ... Watu wengi pamoja na mfalme na mkewe walikusanyika kulisikia Neno la Mungu. Neno la Mungu ni hai, tena lina nguvu, lina ukali kuliko upanga wao wote ukatao kuwili, nalo lilichoma kabisa mioyo ya watu.

Nilipokuwa ninaendelea kuhubiri, Malkia, aliye mwanamke wa kwanza wa mfalme, alianza kuomboleza kwa uchungu. Akasimama, machozi yakamchuruzika usoni, naye akalia sana kwa uchungu akisema: "Ni nani atakayeniokoa ? Tafadhali unisaidie, moyo wangu una uchungu mwingi, mimi ni mtu mwenye mashaka na huzuni moyoni. Ni nani atakayenisaidia? Ni nani atakyenifungulia kifungo hiki kitisho cha mauti? Nifanye nini? Nyote mwanijua, ya kuwa mimi ni malkia, mke wa mfalme, tena mimi pia ni mmoja wa wanawake wa mkutano wa maombi. Kwa miaka zaidi ya ishirini nimekuwa nikihudhuria Kanisani, walakini mambo hayo yote hayawezi kunisaidia, hayawezi kunifanya huru, dhambi zimenifunga. Mimi ni mlevi, mimi ni mwanamke mwuaji. Mikono yangu

**NI NANI ATAKAYENIOKOA ?**



*Atendaye Dhambi ni wa Ibilisi. 1 Yohana 3:8.*

ni michafu, imejaa dhambi, kwa kuwa ina nguvu kutengeneza tembo, kinywewa chenye laana. Dhambi zimenifunga mikono na miguu nami nimekuwa mfungwa na Jahanum."

Alifululiza kulia kwa uchungu mwingi, hata alipokaa akapaza sauti akisema: "Nisaidie! Nisaidie! Ah, ni nani atakayeniokoa? Ni nani atakayenifungulia minyororo hii ya dhambi? Kwa kweli nampenda Mungu, lakini dhambi hunitawala, dhambi zanikokota chini mpaka Jahanum. Nilimwua mtoto wangu wa kwanza wa kiume, nilikuwa nikimbeba mgongoni nilipokuwa nimelewa, nami katika hali iyo hiyo ya kulewa nilianguka chini na kulalia juu ya kichwa cha mtoto wangu wa kwanza niliyempenda naye akafa pale pale. Tafadhalini mnisaidie, niokoeni na mauti haya. Dini ya kutambikia mizimu haikunisaidia. Ibada ya dini haikunisaidia. Ni nani atakayeniokoa? Ni nani atakayeniokoa?"

Nilimjibu nikisema: "Amani na iwe kwako. Taabu yako ndiyo taabu ya kila mtu. Kitabu cha Mungu, ambacho ni Biblia, chaweza kukupa jibu la kutosha kilio cha moyo wako. Warumi 7:15-25, hutuambia jinsi dhambi zinavyotutawala, pia hutuambia yule atakayetuokoa nazo. 'Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili yangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.'

Hakuna budi kilio hiki kitatoka moyo wa kila mmoja: **'Ole wangu, maskini mimi ni nani atakayeniokoa?'** Kama tukimlilia Mungu, atatupa jibu naye atatuokoa.

## HILI NDILO JIBU

*"Namshukuru mungu kwa Yesu Kristo." Warumi 7:25.*
*"Mwana Akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli." Yohana 8:36.*


Yesu ndiye aliye jibu la maswali yetu yote kuhusu uzima wa milele. Yeye ni jibu la kila swali ulilo nalo. Hakuna wokovu katika jina jingine isipokuwa ni kwa Jina la Yesu litupasalo sisi sote kuokolewa kwalo. Matendo 4:12. Yesu pekee ndiye awezaye kutuokoa tutoke katiba dhambi zetu. Damu yake iliyomwagika Msalabani, hiyo pekee, yaweza kutusafisha dhambi yote. Hakuna dakitari, wala dawa, wala mchawi, wala mtu ye yote, wala mhubiri au kuhani, wala kanisa, atakayeweza kukuokoa hata ukatoke katika dhambi. Yesu pekee, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye

dhambi ya ulimwengu aweza kukuokoa kwa Damu yake na kwa nguvu za Roho wake.

Yesu, Mwana wa Mungu alikuja katika ulimwengu huu kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa. Isaya 42: 6,7. Yesu alisema; 'Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi na wa Ibilisi, walakini kama Mwana (wa Mungu), akiwaweka huru, **mtakuwa huru kweli kweli.'** Yohana 8:34-36. Yesu ndiye ile kweli iwawekao huru.

Yesu Mwana wa Mungu alichukua dhambi zetu zote katika mwili wake mwenyewe juu ya msalaba. Dhambi zako zote zimekongomewa Msalabani. "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Isaya 53:7.

## NAMSHUKURU MUNGU KWA YESU KRISTO



*Huyo ambaye mwana (Yesu) atamweka huru, ndiye atakayekuwa huru kweli kweli. (Yohana 8:36)*

Baraba alikuwa mwenye dhambi mkubwa, maana alikuwa mwuaji aliyehukumiwa kifo. Angalisulubishwa, lakini badala yake Yesu aliubeba msalaba huo ambao Baraba angalikufa juu yake. Yesu Mwana wa Mungu alisulubishwa badala ya Baraba, badala yako, na badala yangu, mwuaji aliwekwa huru kwa sababu mtu mwingine alikufa badala yake kifo alichostahili kufa.

Wewe na mimi tumefanana na yule Baraba. Mshahara wa dhambi ni

mauti, bali kipawa cha Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo. Ukitazama Msalaba wa Kristo kwa imani utajiona mwenyewe jinsi ulivyo, na dhambi zako utaziona zimekongomewa katika Msalaba. Yesu alikufa badala yako juu ya Msalaba ili wewe upate kuishi milele; alimwaga Damu yake ili kuondoa dhambi zako. "Kwa maana jinsi hii Mungu alikupenda hata akamtoa Mwanawe pekee ili usipotee bali uwe na uzima wa milele."

Baada ya kusikia maneno haya yote mke wa mfalme alimwamini Yesu kabisa akatoa moyo wake kwake Yeye aliyekufa Msalabani kwa ajili yake, na kumwaga Damu yake ya thamani ili kumsafisha dhambi zake zote. Alimpa Mungu moyo wake wa dhambi naye Mungu alimpa moyo mpya na kumjaza na Roho Mtakatifu. Pamoja na hayo, Mungu hakumsamehe dhambi zake tu, lakini alimwokoa katika nguvu na utawala wa dhambi. Kwa miaka mingi sasa tangu wakati huo, amekuwa akiishi maisha mazuri, ya ushindi juu ya dhambi, tena yaliyo safi. Yeye sasa hanywi aina yo yote ya tembo, havuti au kunusa tumbako, maisha yake sasa ni safi, naye ni shahidi mwenye furaha wa kuishuhudia kweli, ya kwamba yeye aliye katika Kristo Yesu ni kiumbe kipya kabisa; "Ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya." 2 Wakorintho 5:17.

Nawe pia, msomaji mwenzangu, waweza kuwekwa huru kwa imani katika Kristo Yesu. Yesu alisema: "Njoni kwangu, ninyi **NYOTE** msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Njoo kwa Yesu vile vile kama ulivyo, huko huliko. Umwambie dhambi zako zote na taabu zako. Hawezi kukutupa, kama ukimjia kwa moyo wa unyenyekevu, uliopondeka na wa kuamini. Labda wewe mshiriki wa Kanisa wa muda mrefu, lakini umefungwa dhambini. Njoni kwa Yesu, atakuweka huru mara moja, kama vile alivyomponya mwenye ukoma, na yule aliyekuwa kipofu alimponya pia. Yesu ndiye yule yule awezaye kuponya waliovunjika moyo, naye huweka wafungwa hurru. Yeye husamehe maovu yetu **YOTE** na kuponya magonjwa yetu **YOTE.** Zaburi 103:3.

---

If you have found salvation in Christ, or have been otherwise blessed through our Gospel literature, please let us know. We would like to thank God with you, and remember you further in our prayers. **Our Heart of Man Book can now be downloaded in 480 different languages onto cell phones, tablets, etc from our website www.angp-hb.co.za.**

For **free** Gospel literature, books and tracts in over 540 languages, write to:

**E-MAIL: info@angp.co.za**

**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**

**P.O. Box 2191, PRETORIA, 0001, R.S.A.**

(A Gospel Literature Mission financed by donations)

(Reg. No. 1961/001798/08)